

Mikutano ya Mwaka na ya Msimu wa Spring

Kila msimu wa autumn, Bodi za Magavana wa Mshikano wa Benki ya Dunia na [Shirika la Kimataifa la Fedha \(IMF\)](#) hufanya Mikutano yao ya Mwaka kujadili maswala yanayohusiana na kupunguza umasikini, maendeleo ya uchumi ulimwenguni pamoja na fedha. Mikutano ya Kila Mwaka huwezesha ushirikiano wa kimataifa na kuwezesha Benki na Shirika la Fedha kuwashughulikia vyema zaidi nchi wanachama.

Kama ilivyo destruri, Mikutano ya Mwaka hufanywa Washington kila miaka miwili kati ya mitati na, ili ionyeshe hadhi ya kimataifa ya mashirika hayo mawili, kila mwaka wa tatu mikutano hufwanywa katika nchi nyengine mwanachama. Mbali na mikutano ya Bodi za Magavana, Kamati ya Maendeleo na Kamati ya Kimataifa ya Pesa na Fedha hufanywa rasmi.

Pamoja/ wakati wa mikutano hii, Benki na IMF hupanga baraza kadhaa kuwezesha kujumuika kwa serikali na wafanyakazi wa Benki na IMF pamoja na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (NGOs), waandishi wa habari, na sekta ya kibinafsi. Bila shaka, kila juhudi hufanywa ili kuhakikisha kwamba Mikutano ya Mwaka huwezesha kuwa na baraza imara la kuelezea umma – na kwa kupitia vyombo vya habari - majukumu, nia, na matokeo ya kazi na shughuli za Benki na IMF. Kwa namna hii, Mikutano huchangia vyema sana ukweli na usawa.

Kiasi cha kama watu 10,000 uhudhuria mikutano hii, wakiwemo pia wajumbe kama 3,500 kutoka nchi wanachama wa Benki na IMF, kiasi kama 1000 cha wa wakilishi kutoka mashirika ya habari, na zaidi ya waalikwa na wageni mashuhuri 5,000 haswa wanaotoka kwenye biashara za binafsi, jumua ya mabanki na NGOs. Wafanyikazi wa Benki na IMF pia nao hushiriki katika mikutano pamoja na wakilishi wa maserikali.

MIKUTANO YA MSIMU WA SPRING

Kila msimu wa Spring, [Kamati ya Maendeleo](#) ya pamoja ya Benki na IMF, na Kamati ya Kimataifa ya Pesa na Fedha ya IMF hufanya mikutano ya kujadili maendeleo ya shughuli za Benki na Shirika la Fedha. Mikutano Rasmi ya Benki ya Dunia pamoja na Bodi za Magavana wa IMF hupangwa kuwa wakati wa Mikutano ya Kila Mwaka msimu wa autumn.

Vifaa

Mikutano Ijayo
Wa Mwaka 2003

Kituo cha Taarifa
Spring | Mkwaka

Mikutano Iliyopita

2002 Spring | Mkwaka

2001 Spring | Mkwaka

2000 Spring | Mkwaka

1999 Spring | Mkwaka

1998 Spring | Mkwaka

1997 Spring | Mkwaka

1996 Mkwaka

Vipeuzi vyengine

IMF Nyumbani

Kamati ya Maendeleo

Programu ya Mikutano